

LEO MAANDIKO HAYA YAMETIMIA



Hebu tuendeleo kusimama, mkiweza, tunapoinamisha vichwa vyetu kwa maombi.

Mpendwa Baba wa Mbinguni, tunakushukuru usiku huu kwa hii, nafasi nyingine kuja kuhubiri hii Injili ya Yesu Kristo yenye fahari na ya ajabu. Twa kushukuru kwa kuwa Yeye yungali Yeye yule jana, leo, na hata milele. Twakushukuru kwa ajili ya watu hawa waliokusanyika ndani humu katika wakati huu wa majira baridi na wangali na hamu yao kuu, tukitazamia, tukiamini kuwa kitu fulani kisicho cha kawaida tutapewa kutoka kwa Mungu. Twaja na tumaini hilo, Bwana, katika kila mkutano. Twakushukuru kwa ajili ya ibada za juzi usiku maskanini. Twakushukuru kwa ajili ya ibada hapa jioni iliyopita na kwa ajili ya ibada ya leo maskanini. Sisi sote tunatazamia sasa kile utakachokuwa nacho kwa ajili yetu usiku huu.

² Baba, twajua kuwa watu wote wawezao kusogeza mikono yao wangepungua kurasa za Biblia, lakini kunaye mmoja Pekee Awezaye kuihuisha na iwe iliyo halisi na huyo ni Wewe. Baba, tunakutarajia ufanye hilo usiku huu. Tubariki kwa kila njia. Mioyo yetu imejaa furaha sana kama tunavyoona wakati ukiwadia ambao tutamlaki Yeye uso kwa uso—Yeye yule tunayempenda na kuishi kwa ajili yake miaka hii yote. Waongofu wapya wengi, Bwana, wameletwa. Nikisikia kuwa jeshi kubwa, arobaini au hamsini, watabatizwa katika Jina Lako asubuhi ya leo kutokana na ibada ya usiku uliopita. Ee Mungu, tafadhali endelea, twaomba, hadi kila Mzao aliyechaguliwa asili wa Mungu ameona ile Nuru ya Injili na kuingia zizini.

³ Twakuomba utufiche usiku huu nyuma ya Neno lile; tupofushe kwa vitu vya ulimwengu na uturuhusu tumwone Yesu. Na kuwepo na tukio kati yetu kama la ule Mlima wa Kugeuzwa Kwako usiku huu ili tusimwone mtu ye yote ila Yesu pekee. Twaomba katika Jina Lake na kwa ajili ya utukufu Wake, na thibitisho la Injili Yake. Amina. Na mketi.

⁴ Nitageuza hii maikrofoni, au meza hii, kidogo ielekee upande kidogo tu, ikiwa ni vema, ili nione pande zote mbili za hawa makutano. Nadhani naweza kuzipindua hizi maikrofoni hapa vema. Vema, hebu kidogo.

⁵ Tunawasalimu toka jumba kubwa la hotuba hapa usiku huu, marafiki zetu huko Arizona, California, Texas, na kote nchini Amerika kupitia kwa simu. Hii—hii inaenda kote nchini (ibada hii usiku huu) kupitia kwa simu. Kwa hivyo twatumai kuwa Mungu atatubariki.

⁶ Je, mnasikia nyuma huko kule—jengoni humu upande wa kushoto? Vema, wanaenda sasa kutazama sasa yale mawasiliano ya simu kuona kama yanafanya kazi sahihi.

⁷ Kila mtu ni mchangamfu usiku huu? Vema, hivyo ni vizuri. Upande huu, je? Amina. Nina furaha tele kuona kuwa nyote mmeketi starehe. Na sasa kesho usiku makutano yakizidi kuongezeka, kutakuwako pia simu moja kwa moja—iko usiku huu; nadhani wengine wako huko maskanini. Na kesho asubuhi ibada hazitafanyiwa huko maskanini, kwa kuwa kutakuwa na mpamba—maua akipamba kanisa kwa ajili ya arusi kesho adhuhuri. Nao wamehamisha ibada za asubuhi hadi kwa kanisa la Ndugu Ruddle (mmoja wa wasaidizi wetu) na juu kwa njia kuu hapa-62. Je, imetangazwa? Imetangazwa na likijaa huko, tutawachukua wengine wote na kumtuma mhudumu mwingine huko kwa Ndugu Junior Jackson huko Clarksville. Kusudi la kuifanyia kwa Ndugu Ruddle, ni karibu na hapa nasi twaweza—nasi tulidhani mngepapata hapo kwa urahisi. Na ndipo tutaishughulikia kwa njia fulani. Hakikisha ya kwamba wale wote watakaobatizwa wamefika kesho, nami natumai kutakuwako na wengine mia moja au mbili watakaoongezeka kwa wale watakaobatizwa kesho.

⁸ Na sasa kesho usiku...sipendi kutangaza cho chote utakachonena mbele ya wakati huo, lakini usiku mmoja katika ibada au siku moja, ninataka nihubiri kuhusu Je, *Huyu Melkisedeki Ni Nani?* kwa kuwa ni—ni somo ambalo nadhani tunaishi katika wakati huo ambapo funuo hizi zimekuwa swali katika nyakati zote juu ya, “Je, Mtu huyu ni nani?” Nami naamini kuwa Mungu analo jibu kuhusu Mtu Huyu alikuwa Nani. Wengi walisema kundi la manabii; wengine walisema mfalme fulani; wengine...lakini yapasa kuwe na...kukiwako swali, yapasa kuwe na jibu kwa swali hilo ambalo ni sahihi. Hakuwezi kuwa na swali bila kwanza kuwapo jibu.

⁹ Sasa, tunasadiki kuwa Mungu atatupa baraka usiku huu toka kwa Neno Lake tunapolisoma.

¹⁰ Nanyi mmekuwa...Billy aliniambia niwaambie kuwa mmekuwa na ushirika mwema na watu wa hapa ambao wamekuwa wakiongoza kupangwa magari, na askari na kila kitu. Zidini kuendelea vivyo hivyo; hivyo ni vyema sana.

¹¹ Twatumai kuona wakati (Labda hivi karibuni) ambapo tungeleta hema hapa mjini na kulipiga hapa katika kiwanja cha mpira ambapo tungekaa kwa wakati mrefu zaidi, labda kwa mkutano wa majuma matatu au manne, mfululizo. Na hapa, ni vigumu hata kujuana, na ndipo yatubidi kusema kwaheri na tunaondoka tena. Lakini ningependa kuja na kukaa kwa safari ndefu, wakati mmoja ambapo ungekaa na usimalize kwa usiku mmoja au mbili, lakini kukaa tu na kufundisha mchana na usiku, mchana na usiku, na kuendelea na kuendelea. Labda mtu fulani

aende nyumbani na kulisha kuku kukama ng'ombe, na kurudi juma lifuatalo na kuendelea na ibada, ni-ni napenda hilo. Kwa hivyo Bwana awe nanyi.

¹² Sasa, kabla sijaondoka, labda Jumapili asubuhi au Jumapili jioni, au siku fulani (mojawapo wa ibada hizi), najua ninyi nyote mnangoja kusikia ujumbe kuhusu Kweli ya Ndoa na Talaka, ambao ni moja kati ya shida kubwa za siku hizi. Nami. . . Kwa hakika kama nisimamavyo hapa, naamini kuwa jibu sahihi liko katika Neno la Mungu, nami naamini kuwa hayo. . . hayo ndiyo niliyoahidi kurudi nifanye.

¹³ Sasa nadhani, nikijua. . . Kama nijuavyo, nataka kuwa na ibada nyingine hapa Jeffersonville siku ya Jumapili ya Pasaka, nasi tuta—kwa ibada ya mapambazuko na ndipo Jumapili ya Pasaka; kwa hivyo tutaitangaza hapo kabla na kujaribu na labda kupata ukumbi, ikiwezekana, au mahali fulani, kwa ajili ya Jumapili—labda tuje Jumamosi na Jumapili. Sina budi kuruka kwa eropeni na kurudi, kwa kuwa ni karibu ule wakati. . . Yanipasa nichunguze kwanza daftari niliyo nayo na mojawapo wa utaratibu wa safari ni—ni—niliyo nayo huko California. Na ndipo mara tu baada ya hayo, yanipasa niende—Afrika. Kwa hivyo kuweni karibu na mniombee.

¹⁴ Sasa, usiku huu nataka kuwatazamisha kwenye sehemu ya Neno la Mungu linalopatikana katika sura ya 4 ya Injili ya Luka Mtakatifu—sura ya 4 na nitaanzia kifungu cha 16. Yesu akinena: *Leo Neno hili limetimia masikioni mwenu.*

¹⁵ Sasa, tunataka kutoa toka hapo jambo la mwisho jinsi Neno la Mungu lilivyo na nguvu. Sasa, sisi sote twaweza kutambua mashine lakini inahitaji nguvu ya kuendesha ifanye kazi. Twaweza kutambua muundo wa mtambo (motokaa), lakini kunahitajika zile nguvu zinazoendesha ili kufanya magurudumu yafanye kazi na kuzunguka.

¹⁶ Sasa, Yesu alikuwa amerudi hu—huko Nazareti ambapo Yeye alilelewa. Humu kuendelea Maandikoni hapa twaona kuwa wao walisema, “Tulisikia ulitenda haya na yale huko Kapernaumu; sasa hebu tuone ukiyatenda hapa katika nchi yako mwenyewe.”

¹⁷ Yesu alisema, “Hakuna nabii mwenye kukubaliwa katika nchi yake mwenyewe.” Hakuna budi, hapo ndipo ulipolelewa na ndipo watu wanapokujua. Na pale Yeye alikuwa na jina mbaya kwanza kwa kuzaliwa bila baba wa kidunia. Wao walimwita mtoto haramu—kwa kuwa Mariamu alikuwa na mimba hakika kabla yeye kuolewa rasmi, na Yusufu. Lakini hiyo sivyo; twajua haiko hivyo.

¹⁸ Na, juu ya Andiko hili, kile kilichosababisha mimi, kulitazama, kilikuwa kitu fulani kilichotendeka hivi majuzi huko Phoenix, Arizona. Ilikuwa siku ya mwisho ya ibada ambayo ningehubiri kwa Mkutano wa Kimataifa wa Wafanyi Biashara wa Injili Nzima, na katika mkutano huu kulikuweko

mgeni pamoja nasi aliyekuwa askofu wa Kikatoliki, ambaye yeye yu wa Ushirika wa Kikaldayo wa Kanisa Katoliki la Kimitume—Padre Mkuu John S. Stanley, O.S.D. Yeye ni Askofu mkuu wa maaskofu wa Nchi ya Amerika katika Kanisa Katoliki. Hii ilikuwa kadi yake na-na anwani yake.

¹⁹ Naye alikuwa mgeni wa Wafanyi Biashara Wakristo, nami nilikuwa nimemwona huko siku moja kabla. Na nilipokuwa nikinena Jumamosi usiku, naamini ilikuwa, au Jumamosi asubuhi kwa karamu ya kifungua kinywa, nami—basi nilipokuwa nikinena yeye—yeye aliendelea kunitazama. Niliwaza “Hakika mtu huyo hakubaliani na kila kitu ninachosema.” Na—mwajua, mnge-mngemwona yeye; yeye alikuwa akiinua kichwa chake juu chini, lakini sikujua kile kilichokuwa kikitendeka ndani yake.

²⁰ Jumapili hiyo jioni nilipoinuka kunena, nilikuwa naenda kuchukua somo langu kuhusu *Utungu Wa Kuzaa*—ambapo Yesu alisema kuwa kama mwanamke katika utungu wa kuzaa, yeye ana utungu katika kuzaa. Na pia, nilikuwa naenda kunena tokea hapo kama *Utungu* wa kuzaa, (somo lile), nikisema kuwa ulimwengu uko sasa katika utungu. Ya kale yabidi yaondoshwe ili mapya yazaliwe; kama tu mbegu haina budi kuoza ili itoe uhai mpya. Na jinsi maumivu, utungu, ulivyoupiga ulimwengu katika Vita vya Kwanza vya Dunia. Ulikuwa na utungu mkali sana, kwa kuwa wao walikuwa na hewa ya sumu na vinginevyo na karibu vingeamaliza ulimwengu. Na katika Vita vya Pili vya Dunia ulipigwa tena pigo (maumivu) kali sana, wao walikuwa na baruti na pia bomu ya atomiki. Hauwezi kustahimili utungu mwingine. Tukiwa na haya makombora na mengineyo siku hizi, vita moja zaidi itaivurumisha angani, kwa kuwa sasa utakombolewa na kutakuwako dunia mpya. Biblia ilisema kutakuwako.

²¹ Chini ya Ujumbe wa kila nabii Israeli ilipata utungu, kwa kuwa hawa manabii wangetokea baada ya wanatheologia na wahubiri kuliweka kanisa lote katika hali ya dhehebu. Na nabii huyo atokeapo akiwa na “BWANA ASEMA HIVI”, wao walitikisa makanisa hayo nalo likawa na utungu. Mwishowe likawa na utungu ulioendelea hadi lilipomzaa Mwana wa Injili aliyekuwa Neno lililofanyika mwili.

²² Kwa hivyo kanisa hakika liko katika utungu usiku huu tena kwa ajili ya kumzaa Mwana yule—Mwana wa Mungu kurudi tena. Wanatheologia wetu, miongozo yetu yote, madhehebu yetu yote yameoza toka chini yetu. Kwa hivyo sisi tuko katika utungu na Ujumbe toka kwa Mungu kila mara hilitupa kanisa katika maumivu zaidi. Lakini baada ya muda mchache litamzaa bibi—arusi atakayemleta Yesu Kristo kwa Bibi—arusi Wake.

²³ Na ndipo, nikiwaza kuwa mtu huyu alikuwa hajakubaliana nami sana nilipoinuka kunena Ujumbe huu, nilifungua katika Biblia yangu kupata ukurasa ule, na mke wangu alikuwa

amenipa Biblia mpya kama zawadi ya Krismasi. Biblia yangu ya kale ilikuwa na umri wa karibu miaka kumi na mitano, na ilikuwa karibu imeraruka vipande-vipande. Kurasa zile, kila wakati ningeifungua, zingepeperushwa toka humo—lakini nilijua tu pa kupata kila Andiko. Kwa hivyo nilikuwa nimeisoma Biblia hiyo kwa makini, na nilikuwa tu nimechukua ile mpya kwa kuwa ile nyingine ilionekana imekwisha kuchakaa sana kwenda nayo kanisani.

²⁴ Na nilipoanza kufungua katika Injili ya Yohana Mtakatifu, ambapo Andiko hilo lilionekana, nilianza kusoma ile sura ya 16, na kifungu kile nilikuwa nikikitafuta hakikuwepo mle! Kwa hivyo nilidhani, “Ajabu hii.” Nikarudi nyuma tena; bado hakikuwepo. Na Ndugu Jack Moore toka Shreveport, Louisiana, rafiki wangu mkuu, yeye alikuwa ameketi pale. Nilisema, “Ndugu Jack, je, hicho si kinapatikana katika Injili ya Yohana Mtakatifu 16?”

Yeye alijibu, “Naam!”

²⁵ Na huyu kasisi wa Katoliki aliinuka toka kwa kiti chake, toka kwa kundi la karibu wahubiri wapatao mia moja walioketi jukwaani, akaondoka akaja karibu nami, akiwa amevalia joho lake rasmi na mavazi na misalaba na vinginevyo, na akaja karibu nami, yeye akasema, “Mwanangu, kuwa imara. Mungu yu karibu kutenda kazi.”

Nami niliwaza, “Askofu wa Katoliki kuniambia hayo!”

²⁶ Yeye alisema, “Isome kutoka kwa Kitabu changu.”

²⁷ Nami nilikisoma Kifungu kile toka Kitabuni mwake, na nikapata somo langu na kuendelea; nikahubiri mahubiri yangu.

²⁸ Baadaye, nilipomaliza, yeye aliinuka baada ya mimi kuondoka na kusema, “Kuna jambo moja ambalo yapasa litendeke. Baada ya hilo, kanisa lapaswa kutoka katika mchafuko lililomo, au yatupasa kuondoka mchafukoni ule kanisa lililomo.” Kwa hivyo, moja au lingine.

²⁹ Na ni—nilikuwa njiani kuelekea nyumbani (huko chini Tucson) jioni hiyo, watoto walikuwa waakililia sambusa nami nilisimama kununua sambusa katika kituo kidogo. Na mke wangu alisema, “Bill, sijapata kuwa na wasiwasi hivyo maishani mwangu mwote kukuona wewe umesimama juu pale ukiburuga-buruga katika Biblia hiyo.” Kasema, “Je, si ilikufanya uwe na wasiwasi?”

³⁰ Nilisema, “Hapana!” Nilisema, “Nilijua kilikuwa ndani humo mahali fulani; wao hawakuingiza ukurasa huo ndani. Ni kosa la uchapishaji.”

Naye alisema, “Kudhani kuwa nilikupa Biblia hiyo. Ilionekana kama kwamba kila jicho humo lilinitazama.”

Nami nilisema, “Vema, hungezuia hilo. Hilo lilikuwa kosa la uchapishaji wa Biblia.” Nilisema, “wao hawakuweka ukurasa huo humo.”

³¹ Vema, niliifikia chini na kuitazama tena. Kamili tu kama iwezavyo kuwa, lakini sura ya 16, katika sehemu—sehemu yake karibu inchi tatu toka chini, kuendelea kwa ile sura ya 17, upande wa pili u vivyo hivyo, na kwa kuwa ilikuwa Biblia mpya, hizo kurasa mbili zilikuwa zimeshikamana pamoja sana, nami nilikuwa nikisoma toka kwa sura ya 17 badala ya ya 16.

“Vema,” Nilisema, “sawa. Lina kusudi fulani.”

³² Na dhahiri tu kama vile ungesikia sauti yo yote, Sauti ilinijia na kusema, “Yeye alingia Nazareti hapo alipolelewa na akaingia katika sinagogi kama ilivyokuwa desturi Yake. Na kuhani akampa Chuo asome, naye akasoma Isaya 61. Naye alipokisoma kile Chuo, akaketi chini, na kumrudishia kuhani Biblia, kile Chuo, na akaketi chini. Na macho yote ya makutano yalimtaazama Yeye, *na maneno ya thamani yalitoka kinywani Mwake*, na Yeye akasema, ‘Leo Maandiko haya yametimia.’”

³³ “Leo Maandiko haya yametimia.” Jinsi Maandiko yalivyo sahihi! Ikiwa utachunguza hili katika Isaya 61:1-2 ndipo ambapo Bwana wetu alikuwa akisoma kutoka—Isaya 61:1-2. Lakini katikati ya kile kifungu cha pili cha Isaya 61, Yeye alikoma inaposema, “Roho ya Bwana i juu yangu kutangaza mwaka uliokubaliwa.” Ndipo Yeye alikoma. Kwani? Ile sehemu nyingine, na siku ya kisasi, haikuhusika na kule kuja Kwake kwa kwanza, lakini kule kuja Kwake kwa pili! Mwaona, haikuhusika pale; jinsi Maandiko yasivyofanya kosa. Hayo kila mara yako kamili. Yesu alikomea tu ambapo Maandiko yalikomea, kwa kuwa hayo ndiyo hasa yale yalihatijika kuthibitishwa katika siku Zake.

³⁴ Sasa, na kuja huko kwa kwanza. . . Kuja kule kwa pili Yeye ataleta hukumu juu ya dunia, lakini si wakati huo. Yeye alipaswa kuhubiri “mwaka uliokubalika.”

³⁵ Tazameni, yule Masihi, akisimama pale jukwaani kujitambulisha Mwenyewe na lile Neno la Ahadi kwa wakati huo. Ajabu vipi—yule Masihi akisimama mbele ya kanisa! Na tazama haya maneno ya thamani, Yeye asemapo hapa, “Kuhubiri mwaka uliokubaliwa.”

³⁶ Ule mwaka uliokubaliwa, kama tujuavyo kama wasomaji wa Biblia, ulikuwa ule mwaka wa Sikukuu; huo ambao watumwa wote na wafungwa, kama ilivyokuwa. . . wamechukuliwa mateka, nao walihatijika kutoa mwana kulipa deni, au binti kulipa deni, nao walikuwa utumwani. Haijalishi wamekuwa utumwani kwa miaka mingapi au walihatijika kukaa pale mwaka huo wa Sikukuu ulipofika, parapanda ilipolia kila mtu alifanywa huru ikiwa alitaka kuwa huru. Yeye alikuwa huru; yeye hakuwa mtumwa tena.

³⁷ Lakini ikiwa ulitamani kubaki mtumwa, basi ilikubidi upelekwa hekaluni, usimame karibu na kizingiti cha hekalu, nao walichukua msharasi na kutoboa shimo masikioni mwako. Na ndipo ilikupasa kumtumikia huyo mwenye watumwa siku zako zote.

³⁸ Ni mfano kamili jinsi gani wa ile Injili ya Yesu Kristo. Unapohubiriwa, ule wakati uliokubalika na wakati wa Sikukuu, mtu ye yote, haijalishi u nani, u wa rangi gani, u wa dhehebu gani, umejizamisha kilindi gani dhambini, au shida yako ni nini, waweza kuwa huru usikiapo ile—ile parapanda ya Injili ya Mungu ikilia! Wewe u huru! Lakini ukiupa Ujumbe kisogo, na kukataa kuusikia, tazama, ulitobolewa sikio na msharasi. Hilo lamaanisha kwamba, umeruka mpaka kati ya neema na hukumu na hutasikia Injili tena! Hutaendelea tena; lazima uwe mtumwa kwa dhehebu uliomo maishani mwako mwote, ukikataa kusikia ule mwaka uliokubaliwa.

³⁹ Sasa, ile sehemu nyingine yake, kama nilivyosema, haikuhitajika ijibiwe, kwa kuwa Masihi huyu ajaye, wakati wa sasa ni wakati ambapo Yeye ataleta hukumu.

⁴⁰ Basi, ingewezekanaje wale watu wasiweze kuona Yeye alikuwa nani? walilikosaje? Ingewezekanaje wakati ilikuwa imejulikana dhahiri na kuonyeshwa? Wangekosaje kuona wakati Yeye... ni Neno jinsi gani! Wazia hilo! “Leo Maandiko haya yametimia machoni penu!”

⁴¹ Nani alisema hayo?—Mungu Mwenyewe, aliye mfafanusi wa Neno Lake Mwenyewe. “Leo Maandiko haya yametimia.” Yule Masihi Mwenyewe, akisimama mbele ya makutano na akisoma neno toka kwa Biblia linalomhusu Yeye Mwenyewe, na ndipo akasema, “Leo Maandiko haya yametimia,” nao bado walishindwa kulifahamu.

⁴² Ingekuwa msiba jinsi gani, lakini imetendeka. Imetendeka mara nyingi. Ingetendekaje? Hakika, kama ilivyofanyika nyakati zingine, kwa kuamini mafafanuzi ya Neno ya watu. Hiyo ndiyo ilisababisha hayo. Wale waamini katika siku hizo (waliojiita waamini) walikuwa wakichukua mafafanuzi yale makuhani walikuwa wamesema kuhusu Maandiko. Kwa hivyo Yesu akiwa hana cheo cho chote au kuwa chamani mwao, Yeye alifukuzwa toka kwa kundi lao. Na kwa hivyo, wao hawangejitambulisha naye, kwa kuwa Yeye alikuwa tofauti nao. Ule Utu wa Yesu Kristo ulikuwa wa kipekee hivi kwamba, hukuna ye yote angekoswa kuona huyo alikuwa yule Mwana wa Mungu, kwa kuwa Yeye alikuwa kitambulisho kamili cha Maandiko yale yaliyoandikwa kumhusu! Njia ile Mkristo ye yote ajulikanayo—maisha yake yanatambulisha jambo lile lile Wakristo wapaspwalo kutenda.

⁴³ Yeye angesimama pale na kusema, “Leo Maandiko haya yametimia machoni penu!” Ni dhahiri jinsi gani! Ni wazi vipi,

na hali watu wale walielewa vibaya Kwa nini?—ni kwa sababu wao walichukua mafafanuzi maagizo ya kuhani waliyekuwa wakimsikiza. Na historia kila mara hujirudia yenyewe, na Maandiko huwa na maana zaidi ya moja na ufunuo zaidi ya mmoja!

⁴⁴ Kwa kuwa ni kama tu isemavyo katika Biblia “Toka Misri nilimwita Mwanangu” (ikitaja kuhusu Yesu). Tazama kandoni mwa karatasi kuhusu hilo na utatambua kuwa pia linamtaja Yakobo—Andiko lile lile. Yesu alikuwa Mwana Wake mkuu sana. Yakobo alikuwa mwana Wake ambaye Yeye alimwita toka Misri, ambapo kumbukumbu ya Scofield na kumbukumbu zingine zinanena juu yake, kwa kuwa hilo ndilo Andiko ililokuwa ikitaja, ili iwe na jibu mara mbili. Ilikuwa na jibu kwa Yakobo aliyeitwa atoke na kwa Yesu aliyeitwa atoke.

⁴⁵ Na ndivyo ilivyo leo! Ni kwa kuwa sisi tuko katika msukosuko mwingi kama tulivyo, na watu hukosea kuona ile Kweli ya Mungu, ni kwa kuwa kuna mafafanuzi mengi sana yaliyotengenezwa na wanadamu ya Neno la Mungu! Mungu hahitaji mtu ye yote afafanue Neno Lake! Yeye ni Mafafanusi Wake Mwenyewe!

Mungu alisema mwanzoni, “Na iwe nuru,” na ikawa nuru. Hilo halihitaji ufafanuzi.

Yeye alisema, “Bikira atazaa,” naye alifanya hivyo. Hilo halihitaji ufafanusi wo wote.

⁴⁶ Wakati—Ufafanuzi wa Mungu wa Neno Lake ni wakati Yeye alithibitishapo na kulihakikisha kuwa li hivyo! Huo ni ufafanuzi Wake—kwa kulifanya litimie! Hivyo ndivyo ufafanuzi wa Mungu ulivyo, ni Yeye afanyapo Neno Lake kutimia; Yeye anakufafanulia wewe.

⁴⁷ Kama hakukuwa na nuru na akasema, “Na iwe nuru,” na ikawa; hilo halihitaji mtu ye yote kulifafanua. Lakini tunapata taratibu za wanadamu zikichanganywa nalo. Na ufanyapo hivyo, una-unalitoa mahali pake. Kila wakati imekuwa hivyo.

⁴⁸ Lakini bado nawaza jinsi lilivyokuwa la kushangaza. Liwazie! Yule Masihi! Mbona wao walishindwa kumtambua Yeye?—kwa sababu viongozi wao wenyewe waliopaswa kumjua Yeye, ambao walipaswa wawe wameelimika vilivyo Maandikoni, ambao walipaswa wawe wakielewa Maandiko, walimdharau Mtu huyu na kusema, “Kwanza, Yeye ni mtoto haramu.” Sisi hatungeamini hilo. Miaka mingi baadaye hatuamini hilo; tungekufa kusudi tuseme Yeye alikuwa Mwana aliyezaliwa na bikira! Na siku moja itakuwa kwamba mambo yale tuonayo Yehova akifanya leo, wanadamu kwa nyakati zijazo, kama zitakuwapo, watakufa kwa ajili ya jambo hili tunaloongea leo. Itakubidi ufanye hivyo ile chapa ya Myama ijapo, na hutaruhusiwa kuhubiri Injili hivi.

⁴⁹ Wakati muungano mkubwa wa makanisa unakusanyika, ambao u tayari hivi sasa kwa ajili ya kanisa la ulimwengu, itakupasa utie ushuhuda wako muhuri kwa maisha yako kwa ajili ya hili. Yakupasa uamini sasa. Ikiwa makuhani wale waliomhukumu Yeye wangefufuka, hawangemhukumu.

Lakini unasema, “Kama ningalikuwa pale, ningefanya *hili na lile*.”

Vema, hilo halikuwa kwa ajili ya wakati wako, lakini huu ni wakati wako! Huu ndio wakati!

Mwasema, “Vema, kama angekuwa hapa . . .”

⁵⁰ Biblia yasema ni Yeye yule jana, leo, na hata milele—Yeye—yule; kwa hivyo Yeye yuko hapa. Lakini Yeye yuko hapa . . . Jinsi ulimwengu umestaarabika na kuwa mkuu na kuelimika zaidi, Yeye yuko hapa katika hali ya Kiroho, ambayo hawawezi kuua au kuweka mautini. Yeye alikufa mara moja; Yeye hawezi kufa tena. Yeye alipaswa kufanyika mwili ili Mungu awekwe mautini katika mwili kwa ajili ya dhambi. Lakini wakati huu Yeye hawezi kufa kamwe; Ni yule Roho Mtakatifu.

⁵¹ Sasa, jinsi ya kuwaza kuwa wao walikuwa na mambo hayo dhidi Yake. Jambo lingine, kuwa Yeye hangejiunga na vyo vyote vya vyeo vyao. Ndio mwaona, hilo bado lilimfanya Yeye kuwa mtu mbaya. Yeye hakujiunga na—na, madhehebu yao, hangejiunga na ukuhani wao, na hangekuwa na lo lote na hayo. Na ndipo zaidi ya hayo yote, alijaribu kuyabomoa yale waliyoyajenga!

⁵² Yeye aliingia hekaluni. Twamwita Mtu mpole; Yeye alikuwa vile, lakini mara nyingi twakosa kufahamu upole ni nini. Yeye alikuwa ni Mtu mwenye huruma, lakini twashindwa wakati mwingine kufahamu *huruma* ni nini. Huruma ya kibinadamu sio *huruma*, lakini *huruma* ni kutenda mapenzi ya Mungu. Yeye alipitia karibu na birika ya Bethzatha, pale malangoni; pale kulikuwako watu, makutano ya wote. Makutano ya watu si hesabu fulani, lakini kulikuwako wingi wa watu—viwete, vipofu, vilema, waliopooza. Na Yeye kila wakati aliwahurumia watu, na alimwendea tu mtu mmoja pekee aliyekuwa si kilema, kiwete, wala aliyepooza. Labda huenda alikuwa na ugonjwa wa kuzimia roho; labda alikuwa na maradhi madogo yaliyokuwa hayaponi; yeye alikuwa nayo kwa miaka thelathini na minane. Haungemsumbia, haungemwua. Yeye alikuwa amelala kwenye machela.

Naye alisema, “Wataka kuwa mzima?”

⁵³ Na mtu yule akasema, “Sina ye yote wa kunitia majini, lakini wakati ninapokuja mimi, naam, mtu mwingine hushuka mbele yangu.”

Waona, yeye angetembea; angeona; angejisongeza hapa na pale, lakini alikuwa tu mdhaifu.

⁵⁴ Na Yesu alimwambia, “Simama! jitwike godoro lako, na uende nyumbani kwako!” Na walimswali Yesu juu ya hilo. Kwa kuwa ninyi mwakumbuka Maandiko yalisema hivi . . .

⁵⁵ Si ajabu. Kama Yeye angekuja Jeffersonville usiku huu na kutenda jambo hilo, wao bado wangeongea tu kumhusu Yeye. Lakini kumbuka, Yeye alikuja kutenda jambo moja—nalo ni mapenzi ya Mungu. Sasa hayo yanapatikana katika Yohana Mtakatifu 5:19; utapata jibu lile. Yeye alisema, “Amini, Amin nawaambieni, Mwana hawezi kufanya lo lote Mwenyewe ila lile Yeye aonalo Baba akitenda, hilo Mwana analitenda.”

⁵⁶ Sasa, wao wangepaswa kujua kuwa hilo lilikuwa ni thibitisho lile lile la ule unabii wa Musa. “Kwa kuwa Bwana Mungu wenu atawaondokeshea nabii mfano wangu.”

Tazama alipomwona mtu yule yeye alisema . . . Yesu alijua kuwa mtu huyo alikuwa amekuwa hivyo kwa miaka mingi. Yeye akiwa Nabii, alimwona mtu yule kwa hali hiyo na akaenda chini pale na kupunga—kupitia kati ya watu hao, akipenyeza kati ya kundi hadi Yeye akampata mtu fulani. Akapitia karibu na mtu aliyelemaa, aliye kiwete, kipofu, na aliypooza, bali mtu aliyejawa na huruma, lakini huruma ni kutenda mapenzi ya Mungu.

⁵⁷ Sasa, twamwona Yeye, kwa sababu hangeungana nao, na kutokuhusiana na vyeo vyao, ndipo Yeye alikuwa mtu aliyetupwa. Yeye hangekuwa na lo lote . . . Zaidi ya hayo Yeye alikwenda hekaluni siku moja. Mtu yule aliingia humo na kuona nyumba ya Mungu imeoza tu kama siku hizi. Wao walikuwa wakiuza, wakinunua, wakibadilisha pesa, naye akageuza meza zao za pesa, akachukua kamba na kuzisokota na kuwachapa wale wabadili fedha toka mle hekaluni na kuwatazama kwa hasira! Na kusema, “Imeandikwa [Haleluya!], nyumba ya Baba Yangu ni nyumba ya sala nanyi mmeifanya kuwa pango la wanyanganyi! Nanyi, kwa mapokeo yenu, mmezitangua amri za Mungu.”

⁵⁸ Jamani, kundi kama hilo lingemwamini? La, bwana! Wao wamepakwa matope ya vyama na machafu ya siku hizi hata wakagandamizwa kidini sana hadi hawangesikia mawimbi ya nguvu za Mwenyezi Mungu! Si ajabu yule mwanamke angemvua vazi Lake na aponywe, na mwanajeshi mlevi angemtemea mate usoni Mwake na asione nguvu zo zote! Yategemea jinsi unavyoiendea; yategemea unachotafuta. Uendapo kanisani yategemea ni nini unachotafuta.

⁵⁹ Sasa, twamwona Yeye amesimama pale. Bila shaka watu walikuwa wamemwonya Yeye—walimwonya—makuhani walikuwa wamewaonya watu, “Sasa yeye yuaja hapa Sabato ijayo, na akija msimsikize. Sasa, huenda ukaenda na kuketi hapa, lakini usisikie yale yeye asemayo, kwa kuwa yeye si wa kundi letu. Yeye ni aliyekataliwa. Hana kadi ya ushirika;

hata hana kijikaratasi cha dhe—dhehebu. Yeye hana kitu kama hicho.”

“Yeye ni nani?”

⁶⁰ “Kijana fulani mkorofi aliyezaliwa chini pale mwana haramu nyumbani mwa seremala ambaye mama yake alipata mimba kabla hawajaoana, nao wanajaribu kuficha hilo kwa kutumia jambo la kimbinguni. Twajua kuwa Masihi ajapo yeye atapitia kwenye vijia vya Mbinguni na kumwendea kuhani wetu mkuu na kusema, “Niko hapa, Kayafa.”

⁶¹ Lakini twaona kuwa yeye hakulifanya hivyo, kwa kuwa haikuandikwa katika Neno hivyo! Zilikuwa ni desturi za wanadamu zilizowafanya waamini hivyo. Na Neno lilisema Yeye angekuja jinsi alivyokuja! Hapo Yeye alisimama, akisoma Neno na akiwaambia, “Leo Maandiko haya yametimia machoni penu,” na huku walishindwa kumwona Yeye au hawakumtambua Yeye, kama walivyofanya katika nyakati zingine zote.

⁶² Nuhu angesema jambo lile lile siku ile aliyoingia safinani na mlango ukafungwa. Musa angefungua dirisha hilo juu ya safina, akatazama makutano (kumbuka, Mungu alifunga mlango ule) naye angesema, “Leo Maandiko haya yametimia machoni penu.” Lakini ilikuwa imechelewa sana kwao wakati huo. Yeye alikuwa amehubiri miaka 120 akijaribu kuwaingiza katika mtumbwi huo aliokuwa ameujenga, akiwaambia kuwa Maandiko yalisema BWANA ASEMA HIVI kutanyesha! Lakini, wao walingoja sana. Lakini Nuhu angesema hilo kwa urahisi—“Leo, siku hii, Maandiko yale yametimia.”

⁶³ Musa, siku ile ile ambayo ile Nguzo ya Moto iliwashukia kwenye Mlima Sinai na kutoa ushahidi kwa ushuhuda wake, Musa angesema, “Leo Maandiko haya yametimia.”

⁶⁴ Musa, mwajua, alikuwa mtu aliyeitwa na Mungu, nabii. Na alipokuwa akiitwa, awe nabii, ilimbidi yeye awe na ujuzi wa kimbinguni ili awe nabii. Ilimpasa kukutana na Mungu uso kwa uso na kuongea Naye. Na jambo lingine, yale yeye aliyosema ilibidi yatimie au hakuna ye yote angenwamini. Kwa hivyo, hakuna mtu aliye na haki ya kujiita hivyo, hadi ameongea uso kwa uso na Mungu nyuma ya jangwa mahali fulani, ambapo yeye alikutana na Mungu Mwenyewe! Na makafiri wote ulimwenguni hawangemshawishi alitupilie mbali; yeye alikuwa pale, naye alijua ilitendeka. Kila Mkristo apaswa awe na ujuzi huo kabla ya kusema lo lote kuhusu kuwa Mkristo—ujuzi wako mwenyewe!”

⁶⁵ Niliongea na mpwangu muda mchache uliopita, kijana mdogo Mkatoliki, aliyesema, “Mjomba Billy, nimekimbia huku na huko nikienda kila mahali nikijaribu kupata kitu fulani!” Usiku baada ya usiku, kabla mkutano huu kuanza, yeye amekuwa akilia, na wakati wa usiku yeye amekuwa akiota ndoto ya kuingia, akikimbia madhabahuni (panapohubiriwa) na kufanya maungamo kuwa amekosa.

66 Nilisema, “Melvin, haijalishi unakwenda wapi, unajiunga na makanisa mangapi, unatamka ‘Mariamu Mtakatifu’ ngapi, au unapata baraka ngapi toka kwa mwanadamu, yakupasa uzaliwe mara ya pili kwa Roho wa Mungu! Ndilo jambo pekee litakalotosheleza moyo wa mwanadamu.”

67 Ni—ninajua wana badiilisho siku hizi la kuzaliwa mara ya pili—wanasolimiana kwa mikono na mhubiri na kuandika jina lako kitabuni. Lakini marafiki, hayo ni kanuni ya mafundisho ya sharti! Si Kweli ya Biblia! Kama ingekuwa, Matendo ya Mitume katika sura ya 2 ingesomeka hivi: “Hata ilipotimia Siku ya Pentekoste, mchungaji akajitokeza na kusolimiana kwa mikono na watu.”

68 Lakini ilisema, “Hata ilipotimia Siku ya Pentekoste (wakati wa kuanzishwa kwa kanisa), kukaja uvumi toka Mbinguni kama uvumi wa upepo ukienda kasi, ukaijaza nyumba yote waliyokuwa wameketi!”

69 Hivyo ndivyo jinsi Roho Mtakatifu alivyokuja mara ya kwanza; hivyo ndivyo amekuja kila wakati tangu wakati huo! Yeye ni Mungu na habadiliki.

70 Naam hukwaza watu. Wao husema, “Huyo alikuwa kwa wakati mwingine.” Vema, ni Yeye yule jana, leo na hata milele. Kila wakati kanisa lilipowahi kupokea Roho Mtakatifu, kila mara huja kama alivyokuja mara ya kwanza, chini ya amri ile ile ya daktari—Matendo 2:38. Haibadiliki; na haitabadilika kamwe.

71 Kama amri ya daktari kwa ugonjwa, yeye ataandika maagizo fulani kwa ajili ya ugonjwa (daktari hufanya hivyo), na kuwapelekea wengine wasiofuzu, watoe dawa, anaweka nyingi ya dawa inayoharibu sumu, itakuwa dhaifu sana na haitakufaidi cho chote. Akiweka sumu nyingi sana ndani yake, itakuuwa. Lazima iandikwe tu kulingana na daktari. Na maagizo ya daktari ya jinsi ya kumpokea Roho Mtakatifu yametolewa kwetu na Dk. Simoni Petro katika siku ya pentekoste!”

72 Nitawapa amri ya daktari: “Tubuni kila mmoja wenu na mbatizwe katika Jina la Yesu Kristo kwa ajili ya ondoleo la dhambi, nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu, kwa kuwa amri hii ya daktari ni kwa watu walio mbali na kwa wote watakoitwa na Bwana Mungu wetu!” Amri ya milele ya daktari.

73 Musa alikuwa amepata ujuzi huu. Yeye aliingia nchini na kuanza kuwaambia watu, “Nilikutana na Nguzo ya moto. Ilikuwa katika kichaka kilichokuwa kikiwaka, na Yeye aliniambia niwaambie, “MIMI NIKO AMBAYE NIKO. “Telemka chini, nitakuwa pamoja nawe. Chukua fimbo iliyo mkononi mwako na uinue juu ya Misri; cho chote atakachohitaji kitatendeka!”

Vema, labda baadhi ya makutano walisema, “Upuzi!”

⁷⁴ Lakini walipoona jambo halisi la hili liki—likitimia, hawangejizua tena. Walijua yeye alitumwa na Mungu.

⁷⁵ Basi ikiwa Musa alisema yeye aliona hilo na kulishuhudia kuwa Kweli, basi Mungu apaswa, kama hiyo ni Kweli, kutambulisha na kuthibitisha neno la mtu huyo, Kweli! Naam.

⁷⁶ Kama Yesu alisimama pale na kusoma siku hiyo, “Leo Maandiko haya yametimia mbele yenu,” Mungu lazima afanye Neno hilo litimie!

⁷⁷ Twasimama hapa usiku huu na kusema kuwa Yesu Kristo ni Yeye yule jana, leo, na hata milele! Mungu lazima athibitishe hilo kuwa hivyo kwa kuwa ni Neno Lake! Sasa, hilo lafanyaje?—lahitaji imani na kumwamini Yeye. Lahitaji imani na kuamini Neno Lake kuwa ni Kweli.

⁷⁸ Tazama lililotimia Musa alipowatoa wale wana na wale wote waliomfuata. Wale ambao hawakumfuata walibaki Misri, lakini wale waliomfuata Musa, walipovuka Bahari ya Shamu na kuingia jangwani, Mungu alishuka juu ya Mlima Sinai. Hiyo Nguzo ya Moto iliuwasha moto mlima wote na Sauti ilinena toka mle, na Mungu akatoa zile Amri Kumi! Musa angetembea juu pale mbele ya watu na kusema, “Leo Maandiko niliyowaambia kama Nabii Wake yametimia! Leo, nimewaambia kuwa Mungu alinikuta pale katika kichaka kilichokuwa kikiwaka katika Nguzo ya Moto, na Yeye alisema, ‘Hili lote . . . Hii itakuwa ishara. Utawaleta watu wale hadi papa hapa mahali hapa tena!’ Na pale kuna Mungu katika Nguzo ile ile ya Moto niliyowaambia alikuwamo, ikining’inia pale mlimani. Leo unabii huu umetimia. Hapa Yeye anathibitisha kuwa mambo yale niliyoyasema ni Kweli.”

⁷⁹ Mungu atupe watu zaidi kama huyo, ambao ni waaminifu na wanyofu na wasemao Kweli, ambapo Mungu Mwenyezi angethibitisha kuwa Neno Lake lingali Kweli! Yeye yuangali Yeye yule jana, leo, na hata milele. Mbona Yeye hangelifanya? Yeye aliahidi kulifanya.

⁸⁰ Yoshua huenda alisema jambo lile lile, siku ile ile aliporudi kutoka Kadeshi—Barnea ambapo wao walikuwa wamesafiri mbali sana jangwani. Wao walikuwa na shaka nchi ile kuwa aina ya ile nchi ambayo Mungu alisema ingekuwa, lakini Mungu aliwaambia ilikuwa nchi nzuri; ilikuwa ikitiririka maziwa na asali. Na Yoshua na Kaleb waliokuwa ndio wawili pekee ambao wameamini kati ya wale wengine kumi walioondoka. Waliporudi walikuwa na ushahidi; wao walikuwa na kichala cha zabibu ambazo zingebewa tu na watu wawili wenye nguvu.

⁸¹ Yoshua na Kaleb wangesimama pale na kusema, “Leo Maandiko haya yametimia! Hapa kuna ushahidi kuwa ni nchi nzuri.” Hakika. Kwa nini? “Kuna ushahidi kuwa ni nchi nzuri. Ungepata wapi vitu kama vile huko Misri?” Hapakuwepo mahali kama pale. “Lakini leo Maandiko haya yametimia.”

⁸² Yeye angesema jambo lile—lile lile alipofanya unabii na kusema kuta za Yeriko zingeanguka baada ya wao kuzizunguka mara saba-siku saba, mara saba kila siku. Na walipotembea kuzizunguka hizo mara ya mwisho, kuta zile zilianguka! Yoshua angesimama na kusema, “Leo, yule Jemadari Mkuu wa majeshi ya Bwana aliyeniambia majuma kadha yaliyopita kuwa ingetendeka hivi, leo Maandiko haya yametimia! Kuta zile zilikuwa pale chini mchangani. Njoo. Hebu na twendeni tuutwae; ni wetu.”

⁸³ Leo Maandiko haya yametia. Ajabu vipi, mtu wa Mungu amesimama kwa kitu kilicho sahihi.

⁸⁴ Israeli, pale mtoni wakati ule wangemiliki nchi ile, walivuka. Watafanyaje? Ni mwezi wa nne (Aprili); mafuriko yanakuja, kwa kuwa theluji inayeyuka kule Uyahudi. Lo, jinsi ilivyoonekana kana kwamba Mungu alikuwa jemadari ovyo kuwaleta watu Wake chini pale katika mwezi wa Aprili, wakati Yordani ilikuwa imefurika sana kuliko ilivyowahi kuwa.

⁸⁵ Wakati mwingine...Huenda ningepaswa kukomea hapa kama ningekuwa na wakati wa kuwatolea tu kidokezo kidogo. Wakati mwingine huenda ungeketi nje pale ukiwa na kansa au huenda umeketi pale ukiwa na ugonjwa. Ukiwaza, “Mbona, mimi nikiwa Mkristo, niwe hi—hivi? Mbona mimi niwe nikiketi hivi kama mimi ni Mkristo?”

⁸⁶ Wakati mwingine Mungu huruhusu mambo haya kuwa meusi sana hata huwezi kuona juu, kando—kando, au pengine pote, na ndipo Yeye huja kutengeneza njia kupitia kwayo, ili uweze kusema, “Leo Maandiko haya yanatimia, yale Yeye aliyoahidi kuyafanya.”

⁸⁷ Yeye aliruhusu wana Waebrania kutembea moja kwa moja katika tanuru ya moto. Yeye alisema, “Mungu wetu aweza kutuokoa na tanuru ile ya moto, bali kama siyo, hatutasujudu sanamu yenu.” Wao walipotembea pale kukiwa na harufu ya tanuru juu yao—hakukuwa na harufu ya tanuru, juu yao, wao wangesema, “Leo Maandiko haya yametimia.”

⁸⁸ Danieli alipotoka mle tunduni mwa simba, yeye angesema jambo lile lile.

⁸⁹ Yohana Mbatizaji, baada ya miaka 400 ya mafundisho ya kidini...Si ajabu kanisa hilo lilikuwa katika mchafuko wakati huo. Yeye alipotokea nyikani, pale Yordani, angesimama pale ukingoni, kama alivyofanya, na kusema, “Leo Maandiko haya (Isaya 40) yametimia!”

⁹⁰ Jinsi ningekomea hapa na kuwaambia ninyi yale yule kasisi mzee aliyoniambia. Yeye alisema, “Mwanangu, hukumaliza ujumbe huo.”

Nilisema, “Tulia.”

Yeye alisema, “Wamaanisha kama Wapentokoste, hawafahamu hayo?”

Nilisema, “La.”

Yeye alisema, “Nayafahamu.” Na kasisi wa Katoliki pia. Yeye alisema, “Mbona hukuendelea?”

Nilisema, “Tulia.”

Yeye alisema, “Mungu atukuzwe, nayafahamu!”

⁹¹ Na karibu wakati huo huo Roho Mtakatifu alimshukia dada yake aliyekuwa ameketi pale mkutanoni, naye akainuka akinena katika lugha zisizojulikana na kutoa tafsiri ya jambo lile lile kasisi yule nami tulikuwa tukinena jukwaani! Kanisa lote, mahali pale pote pakazuka shangwe! Na habari zake zikaendelea katika mkutano wa Oral Robert juma lililopita, au majuma mawili yaliyopita, na zikawa ndizo mazungumzo katika mkutano huo. Jinsi kasisi huyo aliyeketi chini ya... Yule Roho Mtakatifu alifunua pale kwa mwanamke fulani (dada yake, naamini ndiye) kuhusu yale yaliyokuwa yakitendeka hapa jukwaani na kufunua jambo lile lile tulilokuwa tukificha!

⁹² Saa ile tunayoishi, leo Maandiko haya yametimia! Leo nuru za jioni zimekuja, nasi twashindwa kuiona.

⁹³ Tazamani, Yohana alisema, “Leo, mimi ni sauti ya mtu aliaye nyikani, kama alivyosema nabii Isaya. Itengenezeni njia ya Bwana!”

⁹⁴ Hawakumfahamu; kauliza, “Lo, wewe ni Yesu—” samahani “wewe ni Kristo”

⁹⁵ Yeye alisema, “Mimi si Kristo.” Akasema, “Sistahili kufungua viatu Vyake, lakini” asema, “Yeye yuasimama miongoni mwenu mahali fulani!” Kwa kuwa yeye alikuwa na hakika kuwa Yeye angekuwa pale. Yeye angekuwako katika siku zake kwa maana Mungu alimwambia angemjulisha Masihi.

⁹⁶ Siku moja kijana Mwanamume alikuja akipitia pale, naye aliona ka—kama Nuru juu yake (Ishara) na yeye akapaza sauti, “Tazama, Mwana-Kondoo wa Mungu. Leo Maandiko haya yametimia mbele yenu!”

⁹⁷ Hakika, katika siku ya Pentekoste, jinsi Petro alivyosimama na kutaja yale Maandiko ya Yoeli 2:38, wakati wao wote walikuwa wakicheka—watu wale. Hawangenena katika lugha zao wenyewe; wao walikuwa wakigugumiza kitu fulani kingine. Biblia ilisema “Ndimi zilizogawanyikana.” Kugawanyika ni ndimi zilizotawanyika, si kusema lo lote, wakigugumiza tu, wakikimbia hapa na pale kama kundi la watu waliolewa.

⁹⁸ Na wao wote walisema, “Vema watu hawa ni walevi; watazameni. Tazamaeni jinsi wanavyotenda—jinsi wao wanawake na wanaume... Hawana adabu” Walivyosema watu wa kidini wa siku hiyo.

⁹⁹ Petro alisimama kati yao, akasema. “Waume na ndugu, ninyi nyote mkaao Yerusalemu nanyi mnaoishi Uyahudi, na ijulikane kwenu kuwa hawa hawajalewa kama mnavyodhani, kuona kuwa ni saa tatu mchana, lakini jambo hili ni lile lililonenwa na nabii Yoeli: “Itakuwa katika siku za mwisho, nitamwagia watu wote Roho Yangu. Leo Maandiko haya yalitimia.” Hakika.

¹⁰⁰ Luther alikuja kwa wakati unaofaa. Wesley alikuja kwa wakati unaofaa. Pentekoste ilikuja kwa wakati unaofaa. Hakuna cho chote kisicho taratibu.

¹⁰¹ Sasa, nawaulizeni kuchunguza wakati na saa tunayoishi sasa na lile Neno lililoahidiwa kwa siku hii. Kama huko nyuma nyakati zingine watu wangesema, “Leo Maandiko haya. . . Leo Maandiko haya. . .” basi na Maandiko ya leo, je? Nini ahadi ya leo? Tumesimama wapi? Tunaishi katika wakati upi, saa inapogonga, ile saa ya kisayansi, usiku wa manane kasoro dakika tatu?

¹⁰² Ulimwengu una fadhaa; kanisa limo kitandani mwa mchafuko. Hakuna ye yote ajuaye wanakosimama. Ni saa ngapi? Maandiko ya siku hizi, je?

¹⁰³ Hali za kanisa—hali za kanisa leo. . . Ulimwenguni, siasa, utaratibu wa ulimwengu wetu, umeza tu kama uwezavyo kuwa. Mimi si mwanasiasa; mimi ni Mkristo, lakini sina shughuli kuongea kuhusu siasa, lakini nataka tu kusema zimeza pande zote mbili.

¹⁰⁴ Nilipiga kura mara moja; hiyo ilikuwa kumpigia Kristo. Yanipasa ishinde. Shetani alipiga kura dhidi yangu, na Kristo alinipigia mimi. Yategemea wapi ninatupa kura yangu. Ninafurahi nilimpigia Yeye. Na ulimwengu useme kile watakacho, ningali naamini kuwa ni Yeye yule jana, leo, na hata milele! Yeye atalithibitisha. Bila shaka atafanya hivyo. Hakika.

¹⁰⁵ Kuongezeka kwa uvunjaji wa sheria—hatia za na watoto. Tazama taifa letu, wakati mmoja ua la dunia. Na demokrasia yetu kuu ilizaliwa nyuma huko na—ule Mkataba wa Uhuru—na ule Mkataba wa Uhuru ulitiwa sahihi, nasi tulipata demokrasia, na babu zetu wa kale na mambo yale waliyotenda. Tulikuwa na taifa kuu, lakini sasa limeza na linabomoka—bomoka na kutikisika na lavunjika, na kujaribu kulipiza watu kodi wapate pesa watume ng’ambo kule kununua urafiki kwa adui. Wao wanazitupa nyuma usoni petu. Vita vya kwanza vya dunia, vita vya pili vya dunia, na hali ukiendelea kwa vile vya tatu. Hakika. Siasa zimeza, zimechafuka—zimeza hadi shinani. Kama tu vile hasa yale Mathayo 24 ilisema ingekuwa. “Taifa litaondoka kupigana na taifa, na ufalme kupigana na ufalme.” Mambo haya yote yatatukia. Hebu tuyakumbuke haya sasa!

¹⁰⁶ Vema, tazameni lingine: kuongezeka kwa uchunguzi wa kisayansi. Sasa, wakati mmoja tu. . . Babu yangu alitumia gari

la kukokotwa na ng'ombe kwenda kumtembelean nyanya yangu. Sasa ni eropleni za jeti au hata mzunguko hadi kwa—hadi anga za juu Sana. Ni kuu. Vipi. . . Nani alisema hili? Danieli 12:4 yasema, “Maarifa yataongezeka katika siku za mwisho.” Twaona saa tunayoishi.

¹⁰⁷ Tazama sasa zile—zile hali za ulimwengu, hali ya sayansi. Na tazama tena leo katika utaratibu wetu wa elimu—sasa msijaribu kukana hili, nina kato za gazeti—kufundisha mambo ya kiume na kike kanisani mwetu—shuleni mwetu juu ya wanafunzi wachanga kujuana kimwili mmoja kwa mwingine kuona ikiwa wanaweza kupata wenziwe ulimwenguni! Naam, bwana.

¹⁰⁸ Je, ni vipi katika ukasisi wetu? Usiku huu nilipata kijikaratasi toka gazetini, huko Los Angeles, California, ambapo kundi la wahubiri (wahudumu wa Baptisti na Presbiteria) waliingiza kundi la walawiti na kufanya ulawiti, wakisema wao walikuwa wakijaribu kuwaleta kwa Mungu, wakati hilo ni mojawapo wa laana za wakati huu—msodoma! Na hata sheria iliawafunga.

¹⁰⁹ Sasa tuko wapi? Utaratibu wetu wote umeoza chini yetu. Nimeona ongezeko la walawiti kote nchini Amerika wameongezeka kati ya 20 na 30 asili mia mwaka uliopita. Wazia hilo! Mwanamume akiishi na mwanamume, kama tu vile walivyofanya huko Sodoma.

¹¹⁰ Kwa uvunjaji sheria—hatia za watoto. Tunaishi katika wakati gani? Leo Neno hili la unabii limetimia.

¹¹¹ Ulimwengu wa kidini, kanisa lenyewe, kanisa lile, kanisa lile lililoitwa litoke (tunaloita kanisa lililoitwa litoke), ule wakati wa kanisa la mwisho, wakati wa kanisa la Kipentekoste—uko wapi? Uko katika Laodikia kama Maandiko yasemavyo.

¹¹² Leo wamelegeza vipingo na wake wao wamevalia tu nusu, wanaume wao wa . . . ni jambo baya sana! Wengine wao wameoa mara tatu au nne, na wako kwenye halmashauri ya mashemasi na kila kitu kinginecho. Wao wamelegeza na kuingiza uchafu, kwa kuwa wao wameketi katika mabaraza na kuchukua nafasi pamoja na ulimwengu. Na leo wana majengo mazuri kuliko waliyowahi kuwa nayo. Mahali pengine mmoja wao anajenga jumba la hotuba la gharama ya dolla milioni hamsini—dolla milioni hamsini!—Wapentekoste! Ilikuwa pembeni chini kule miaka ishirini na mitano iliyopita wakipiga tari. Kasema, “Sisi . . . kwa kuwa . . .” Maandiko yalisema katika Ufunuo 3 kuwa u tajiri. Kasema “Mimi ni tajiri, naketi kama malkia wala sina haja ya kitu.” “Na hujui kuwa wewe u mnyonge, na mwenye mashaka, na maskini, na kipofu, na uchi”—na hujui! Leo Maandiko haya yametimia machoni penu. Amina!

¹¹³ *Amina* maana yake ni iwe hivyo. Sijifanyii mwenyewe amina, lakini namaanisha kuwa naamini kuwa ni Kweli. Leo Maandiko haya yametimia.

¹¹⁴ Kanisa la Kipentekoste liko katika hali ya Laodikia. Lo, wao wangali wakiruka na kupiga makelele na kuendelea wakati muziki unapochezwa. Muziki ukomapo kucheza—au ule mdundo wa kucheza ngoma wengine wao hucheza na kuuita Ukristo—na huo ukomapo, utukufu wote umekwisha.

¹¹⁵ Ikiwa ni kutukuza Mungu halisi, hakuna filimbi za kutosha na nguvu za kutosha ulimwenguni kukukomesha! Wakati kutukuza kweli kwa toka kwa Mungu, hakuhitaji muziki kucheza; kunahitaji Roho wa Mungu kushuka chini; kufanya hivyo! Nao walilisahau zamani, kwa kuwa wao waliweka kipimo cha kipawa cha Roho Mtakatifu kuwa—ishara halisi ni kunena kwa lugha, nami nilisikia pepo na wachawi wakinena kwa lugha!

¹¹⁶ Roho Mtakatifu ni Neno la Mungu ndani yako anayejitambulisha Mwenyewe kwa kukubali Neno hilo. Mbali na hilo hawezi kuwa Roho Mtakatifu. Ikiwa asema ni Roho Mtakatifu na anakana neno la Biblia hiyo, hawezi kuwa ni Roho Mtakatifu. Hiyo ndiyo ishara amini usiamini.

¹¹⁷ Tazama, ishara nyingine kuu. Wayahudi wako nchini mwao, taifa lao wenyewe, pesa zao wenyewe, mwanachama wa Umoja wa Mataifa, wanayo majeshi yao wenyewe; wana kila kitu. Wao wako nchini mwao ambayo Yesu alisema, “Jifunzeni mfano wa mtini.” Wako pale, pale pale taifani mwao. Leo Maandiko haya yametimia.

¹¹⁸ Wayahudi wako nchini mwao—Leo Maandiko haya yametimia. Ule Wakati wa Kanisa wa Laodikia—Leo Maandiko haya (Mathayo 24) yametimia. Ulimwengu uko katika mchafuko (wote kwa jumla), taifa likiinuka na kupigana na taifa, matetemeko ya nchi mahali mahali, vimbunga vikuu vikishuka na kutikisa mataifa na mengineyo, misiba mikuu kila mahali—Leo Maandiko haya yametimia.

¹¹⁹ Sasa, tumeona hali ya ulimwengu. Twaona kanisa la kawaida tu—chama, madhehebu, twaona yalipo. Twaona mataifa yalipo. Nasi twaona kuwa leo ahadi hizi zimetimia. Sasa! Lakini katika siku hizi yapasa kuje Mzao Maalum wa Kifalme wa Ibrahimu. Hivyo ndivyo hasa itakavyokuwa, atakuwa Bibi-arusi wa Kifalme kwa Mwana yule wa Kifalme aliyeahidiwa. Kama nilivyonena usiku uliopita, hatakuwa mzao wa kawaida, atakuwa Mzao wa kiroho. Sharti kuwepo Bibi-arusi wa kiroho atakayeinuka, atakayekuwa Mzao wa Kifalme wa imani ya Kifalme ya wana wa Kifalme wa Ibrahimu. Sharti yeye aonekane katika siku za mwisho, na wakati na mahali ni ahadi aliyopewa kulingana na Malaki 4 (Maandiko yale). Yapasa kuzuke Ujumbe utakaotikisa mioyo ya watu hadi irudie wale baba wa kimitume tena.

¹²⁰ Kutatokea mmoja akiwa na nguvu za Eliya—atakayezuka; mtu wa jangwani atakayejitokeza na atakuwa na Ujumbe

utakaozuka moja kwa moja kurudia Neno tena. Hiyo ni saa tunayoishi.

¹²¹ Basi waza. Sasa, nawaulizeni ninyi katika saa hii, ninyi watu hapa Jeffersonville katika mwaka wa 1933, ile Nuru ya kimbinguni ilishuka huko mtoni siku moja nilipokuwa nikibatiza watu mia tano katika Jina la Yesu Kristo (nilikuwa mvulana wa umri upatao miaka ishirini), ilisemaje, Jeffersonville? Ilikuwa nini huko mwanzoni mwa barabara iitwayo Spring pale, wakati *Courier Journal* (Nadhani lilikuwa lile gazeti la *Louisville Herald*) lilipoandika habari hizo, na zikapitia kwa Associated Press, hadi kule Canada. Dk. Lee Vayle alikata toka gazetini kule Canada mnamo mwaka wa 1933!

¹²² Nilipokuwa nikimbatiza mtu wangu wa 17 chini ya Shahidi huyu (nanyi mwajua mengine juu ya habari hizo), nami nilipokuwa nikisimama pale nikimbatiza huyu mtu wa 17, Nuru, ilishuka chini toka Mbinguni, ikiangaza chini juu ya mahali pale kama nyota iliyoanguka toka Mbinguni. Sauti ilisema, “Kama vile Yohana Mbatizaji alivyotumwa kutangulia kuja kwa kwanza kwa Kristo, Ujumbe wako utatangulia kuja Kwake kwa pili duniani kote.” Leo Maandiko haya yametimia! Asante, Bwana.

¹²³ Leo . . . Mungu aliliahidi. Nini kilitendeka. Leo imeenea kote ulimwenguni. Na Mungu aliposhuka chini pale na kusema hilo (nilipokuwa mvulana mdogo) katika kijiti kilichowaka au kichaka juu pale kikiwaka kwa Nguzo ya Moto—juu pale mahali pa Wathens kule Utica Pike, nikiteka maji nyuma kule katika kibanda kile hadi mahali pa kutengenezea pombe isiyo halali. Mwajua kweli yake.

¹²⁴ Yeye alisema, “Usivute sigara, wala kunywa pombe, wala kuchafua mwili wako, kwa kuwa kuna kazi utakayoifanya uwapo mtu mzima.”

¹²⁵ Nashuhudia hayo kuwa Kweli kwa kuwa niliiona! Na Mungu, kama vile alivyomfanyia Musa, alinena kule chini mbele ya makutano na kusema, “HILI NI KWELI!” Leo Maandiko haya yametimia kati yetu!

¹²⁶ Tazama kile Yeye alisema kuhusu upambanuzi na jinsi ungekuwa, kutoka kuwawekea watu mikono juu yao kujua siri za moyo. Leo Maandiko haya yametimia mbele ya yaya haya macho yetu! Ahadi hizi zilizofanywa.

¹²⁷ Tazama, ahadi hizi zote zimethibitishwa na kutimizwa na Mungu wa Ahadi. Tazama, ikining’inia kule Washington, D.C., usiku huu, ile picha ya yule Malaika wa Bwana. Kama vile George J. Lacy, kiongozi wa upelelezi (F.B.I.) wa sahihi za vidole na hati zilizotiliwa shaka za Serikali ya Nchi ya Amerika, aliichunguza toka Houston, Texas na kusema, “Hiki ndicho Kiumbe Peeke cha Kimbinguni kilichowahi kupigwa picha

ulimwenguni mwote.” Yeye alipaswa kujua; ndiye aliye bora zaidi ulimwenguni kwa hayo.

¹²⁸ Tazama, pale yaning’inia kama Kweli, Nguzo ile ile ya Moto iliyowaongoza nyuma kule Waisraeli jangwani. Inaongoza leo—Uwepo kama ule ule uliotoka Misiri! Leo Maandiko haya yametimia. Mwajua Ujumbe ule ambao Yeye alisema.

¹²⁹ Tazama ono lile la Tucson miaka mitatu iliyopita. Wakati nilikuwa nasimama pale njiani, wakati miaka mitano hapo kabla Yeye alisema, “Siku ile mji huo utakapopigilia kigingi mbele ya lango lile, geukia upande wa magharibi.” Ninyi watu wa maskani ambao mmekuwa hapa mwajua kuwa hilo ni sahihi—wakati huo. Naam.

¹³⁰ Na siku ile yule Bw. Goyne pamoja nao walipokuwa juu pale na kupigilia chini kile kigingi, nilimwambia mke wangu, “Kuna kitu fulani kuhusu hili.”

Yeye akasema, “Ni nini?”

¹³¹ Nami niliingia, nikatazama katika kitabu changu kidogo; ilikuwa pale! Na asubuhi iliyofuata saa nne, nimeketi ndani mle katika chumba changu yapata saa nne, yule Malaika wa Bwana alishuka naye akasema, “Kwenda Tucson. Utakuwa kaskazini mashariki ya Tucson na pale kutakuja Malaika saba katika kundi litakalotikisa nchi yote karibu nawe.” Na kusema, “Utaambiwa toka kule.”

¹³² Wangapi wanaokumbuka hilo hapa, kabla halijatendeka? Kunao watu wanaoketi papa hapa jengoni mumu usiku huu waliokuwa wamesimama papo hapo ilipotendeka, na kusema ile Mihuri Saba ya siri zilizofichwa za Biblia yote zingefunuliwa na kutimiza Ufunuo 10 ya kwamba katika Ujumbe wa Malaika wa Saba mambo haya yetatimia. Leo Maandiko haya yametimia machoni petu! Leo Maandiko haya yametimia.

¹³³ Mwaka jana—nikisimama mahali pale pale (Bw. Wood hapa pamoja nami), tukikwea mlima, katika—akiomboleza juu ya mkewe kuwa mgonjwa; Roho Mtakatifu alisema, “Chukua lile jiwe pale; litupe juu hewani; lirudipo chini sema, ‘BWANA ASEMA HIVI!’ Kutakuwako hukumu itakaogonga dunia. Mwambie kuwa yeye ataona mkono wa Mungu katika muda wa masaa machache yajayo.”

¹³⁴ Nilimwambia Bw. Wood (aliye hapa usiku huu) nami nadhani watu wanane au kumi—au kumi na watano walikuwako pale wakati huo, yalipotendeka asubuhi iliyofuata, ambapo Bwana alishuka kwa upepo wa kisulisuli na kuupasua mlima kutuzunguka, na kukata vichwa vya miti, na kufanya milipuko mitatu na kusema, “Hukumu inaelekea ile pwani ya magharibi.”

¹³⁵ Siku mbili baadaye Alaska ilikuwa karibu kuzama ardhini! Na tangu hapo juu na chini ya pwani zinakomoa hukumu za Mungu dhidi ya “kiambaza cha kiroho!”

¹³⁶ Kuna Pazia ya chuma, kuna Pazia ya Mianzi, na Pazia ya Dhambi! Ustaarabu husafiri pamoja na jua; hata ndivyo na Injili pia. Huja toka mashariki na ilikwenda magharibi kama jua liendavyo, na sasa lko kwenye pwani ya magharibi. Haitaendelea mbele zaidi; ikiendelea mbele zaidi, itakuwa imerudi tena mashariki.

¹³⁷ Nabii alisema, “Kutatokea siku ambayo haiwezi kuitwa usiku wala mchana —siku ya kuhuzunisha, mvua nyingi na ukungu, ya kutosha tu haidhuru—kujua jinsi ya kujiunga na kanisa au kuweka jina lako kitabuni. Lakini kutakuwako Nuru wakati wa jioni. Leo Maandiko haya yametimia!

¹³⁸ Lile lile . . . j-u-a lile lile lipambazukalo mashariki ndilo j-u-a lile lile litualo magharibi. Na M-w-a-n-a yule yule wa Mungu aliyetokea mashariki na kujithibitisha Mwenyewe kama Mungu aliyefanyika mwili ndiye M-w-a-n-a yule yule wa Mungu aliyeko katika kizio cha magharibi cha dunia ambaye anajitambulisha Mwenyewe kati ya kanisa usiku huu—Yeye yule jana, leo, na hata milele! Ile nuru ya jioni ya Mwana imekuja. Leo Maandiko haya yametimia mbele yetu.

¹³⁹ Tuko wapi katika wakati huu wa Ki-Ibrahimu? Tuko wapi katika huu wakati mkuu tunaposimama, saa ile kuu tunayoishi? Maono yote yametimizwa. Vipi jinsi wakati ule kijana mhudumu rafiki yetu hapa, wa kanisa shirika (Junior Jackson), alipokuja akikimbia hadi kwetu usiku mmoja (mimi nikiwa chini pale) na kusema, “Nilikuwa na ndoto, Ndugu Branham, inayonitatiza. Niliwaona ndugu wote wamekusanyika juu ya mlima.” Kisha kasema, “Juu ya mlima huu, ulikuwa ukitufundisha kwa herufi zilizokuwa zimeandikwa, ilionekana kama baadhi ya herufi za kale sana zilizochorwa mwambani. Ulipomaliza, hayo—hayo yalipomalizika, ulituambia, kasema, ‘Njooi karibu,’ nasi sote tukakusanyika.” Kasema, “Ulinyosha mkono kuelekea mahali fulani na ulionekana kama ulichukua, kitu kama mtaimbo na kupiga kilele cha hiyo piramidi ndogo hata ikafunuka. Na ilipofunuka,” kasema, “jiwe gumu lisilo na maandishi juu yake. Nawe ukatwambia tulitazame. Nanyi nyote—sisi sote tukaanza kutazama.” Kasema, “Niligeuza kichwa changu, na mikakuona ukielekea upande wa magharibi haraka iwezekanavyo, kuelekea machweo ya jua.” Wangapi wanakumbuka hayo?

¹⁴⁰ Nami nilisimama pale kwa kitambo kidogo hadi Roho Mtakatifu aliponifunulia. Nilisema, “Biblia nzima, kwa umbali ule ilikuwa imefunuliwa kwa wanadamu kupitia kwa kuhesabiwa haki, kutakaswa, na ubatizo wa Roho Mtakatifu, ule ubatizo katika Jina la Yesu, na mambo haya yote yamefunuliwa, lakini kunayo siri iliyofichika ndani, kwa kuwa Biblia imetiwa mhuri kwa Mihuri Saba. Lazima niende kule niitafute.”

¹⁴¹ Asubuhi hiyo wakati Malaika hao saba waliposhuka chini na kulipua dunia, majabali yaliruka yakipeperuka kila

mahali, wale Malaika saba walisimama pale na kusema, “Rudi Jeffersonville toka kule ulikotoka, kwa sababu ile Mihuri Saba ya zile Siri Saba itafunuliwa.”

¹⁴² Tuko hapa leo, tunafahamu *Uzao wa Nyoka*; katika siku chache, Mungu akipenda, tutafahamu usahihi wa *Ndoa na Talaka* na mambo haya yote ambayo Mungu ameyafunua, kila Muhuri, zile siri, tangu dunia kuwekwa msingi, nasi tumefurahia Uwepo wa baraka Zake. Hiyo ni kweli. Leo Maandiko haya . . .

¹⁴³ Lile gazeti liitwalo *Life* liliandika habari juu yake, “Duara ya siri ya nuru inakwenda juu hewani juu ya Tucson na Phoenix”—katika njia ile ile niliyowaambia yapata mwaka moja kabla haijatendeka, jinsi ingekuwa katika ka—kama umbo lenye pembe tatu. Picha ile inaning’inia kanisani chini pale. Ninyi mliochukua gazeti lile mnayo. Ilikuwa pale vivyo hivyo. Wao walisema lilikuwa maili ishirini na saba juu na maili thelathini upana. Bado hawafahamu ni nini kilitendeka. Lilionekana tu kisiri na kutoweka kisiri.

¹⁴⁴ Na Ndugu Fred Sothmann, Ndugu Gene Norman na mimi tulisimama pale, mashahidi watatu, kama vile ilivyokuwa huko juu katika kilele cha mlima—Petro, Yakobo, na Yohana. Kushuhudia; walisimama pale na kuitazama ilipokuwa ikitendeka na kuona ikifanyika! Iko pale, ikipepea angani mbali sana Pasipo na mvuke, wala unyevu, hakuna cho chote cha kufanya u—ukungu. Lingekuwa pale? Walikuwa ni Malaika wa Mungu wakirudi baada ya Ujumbe wao. Leo unabii wao umetimia kati yenu: Leo Maandiko haya yametimia.

¹⁴⁵ Tazama. Mihuri Saba imefunuliwa, pepo za kisulisuli upande wa Pwani ya magharibi. Sasa, usilikose kama walivyofanya nyuma kule. Sasa, hebu tuyageukie mambo ya siku yetu.

¹⁴⁶ Maandiko yasemaje kuhusu leo na kuhusu wakati tunaishi? Yesu akinena . . . Sitakuwa na wakati wa kuyachukua yote, lakini nataka kuchukua hili moja kabla hatujakoma. Yesu alisema katika Injili ya Luka Mtakatifu ile sura ya 17, kifungu cha 30—Yesu Kristo, yule Neno Mwenyewe (mwaamini hilo?)—Yesu Kristo, yule Neno Mwenyewe aliyefanyika mwili, alinena na kusema jinsi Neno lingekuwa katika wakati wa mwisho, nini ingekuwa ishara ya mwisho wa ulimwengu. Yeye aliwaambia taifa lingeondoka kupigana na taifa, lakini Yeye alisema, “Kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma, ndivyo itakavyokuwa katika Siku ile atakayofunuliwa Mwana wa Adamu.”

¹⁴⁷ Sasa Yesu alipokuja duniani Yeye alikuja katika majina matatu ya Mwana: Mwana wa Adamu (ambaye ni nabii), Mwana wa Mungu, na Mwana wa Daudi. Sasa Yeye aliishi hapa duniani, hakusema kamwe kuwa alikuwa Mwana wa Mungu. Yeye alisema, “Mimi ni Mwana wa Adamu.” Yehova Mwenyewe alimwita Ezekieli katika manabii “Mwana wa Adamu,” kwa kuwa Yeye alihitajika aje kutimiza Maandiko kama nabii!

Musa alisema, “Bwana Mungu wenu atamwondokeshea Nabii kati yenu aliye mfano wangu mimi.” Hiyo ndiyo sababu Yeye hangekuwa Mwana wa Mungu, wakati huo, kwa kuwa Yeye alikuwa Mwana wa Adamu! Neno lilimjia nabii na Yeye alikuwa Neno katika utimilifu wote! Mwana wa Adamu, yule Nabii Mkuu, sio Nabii Mkuu, lakini Mungu Nabii! Ule utimilifu wa Uungu jinsi ya mwili ulikuwa ndani Yake, kwa hivyo Yeye alikuwa Mwana wa Adamu.

¹⁴⁸ Sasa, kwa miaka elfu mbili Yeye amejulikana kwetu kama Mwana wa Mungu, Roho. Na katika ule Utawala wa miaka elfu Yeye atakuwa Mwana wa Daudi, juu ya kile Kiti cha Enzi. Sote twajua hilo tunaoamini Maandiko.

¹⁴⁹ Sasa Yesu alisema tu katika mwisho wa huu wakati wa kanisa tunaishi, kuwa Mwana wa Adamu angefunuliwa tena katika hali ile ile ilivyokuwa huko Sodoma. Tazama jinsi Yeye alivyoitoa kihistoria. Yeye alisema, “Kama ilivyokuwa katika siku, kwanza, za Nuhu, jinsi walivyokuwa wakila, wakinywa, wakioa na kuolewa.” Ndipo Yeye akataja ya pili kutoka mwisho juu ya Mwana wa Adamu katika Sodoma, kwa kuwa hapo Yeye alikuwa akiwashughulikia Wayahudi. Hapa Sodoma Yeye anawashughulikia Mataifa. Pale Yeye aliwazamisha majini katika hukumu. Hapa kuna Mataifa, Yeye aliwachoma wote katika siku za Sodoma. Naam; ulimwengu wa Mataifa uliteketezwa pale.

¹⁵⁰ Na ndivyo itakavyokuwa atakapofunuliwa Mwana wa Adamu. Si maji tena, lakini itakuwa moto wakati huu. Yesu alisoma Mwanzo 23 tunayoisoma, Yeye aliposoma kuhusu Sodoma.

¹⁵¹ Sasa, twakubali hali ilivyonenwa ya—ya—hali ya ulimwengu wa Sodoma, Ulawiti—hali ya Sodoma. Sisi kila mmoja atasema, “Amina” kwa hilo; twaamini hilo. Vema, na hali ya kiroho ya Laodikia, lile kanisa la kawaida, tutasema, “Amina” kwa hilo, na kukubali ishara zao. Twajua kuwa kila ishara iko pale; kanisa liko katika Laodikia, twajua hiyo. Twajua ulimwengu uko katika hali ya Sodoma. Siyo? Tutakubali hiyo. Lakini i wapi, ile Ishara ya Ibrahimu, anayemngojea yule mwana aliyeahidiwa? Hiyo ilikuwa nyingine. Kumbuka, wao walikuwa na Sodoma huko nyuma; wao walikuwa na mjumbe wao. Na Ibrahimu alikuwa na Mjumbe kwake. Ibrahimu alikuwa akingojea siku kwa siku kwa ajili ya—ya jambo ambalo karibu haliwezekani kutendeka—Sara, miaka tisini na yeye, miaka mia moja. Kulingana na ahadi ya Mungu yeye alikuwa bado akingoja. Mbali na kulaumiwa yeye alikuwa akingojea mwana huyo. Mwamini wa Kweli pia angali akingoja huyo Mwana aliyeahidiwa kurudi.

¹⁵² Tazama, kabla tu mwana kufika, kulikuwa na ishara iliyotolewa kwake. Je, si Ishara ile ya kuja kwa Mwana

itafunuliwa kwa yule Mzao wa Kifalme wa Ibrahimu anayemngojea yule Mwana wa Kifalme, kama tu ilivyokuwa kwa baba Ibrahimu kwa ajili ya mwana wa kawaida? Sivyo? Yesu alisema hivyo hapa katika Injili ya Luka Mtakatifu 17:30, kabla ya wakati huu kuja, Mwana wa Adamu angefunuliwa kama Yeye alivyofanya katika siku za Sodoma, kabla ya kuangamizwa kwa Sodoma. Sasa, tunatarajia Ishara.

¹⁵³ Sasa hebu tuchukue...?...hali za wakati kama ilivyokuwa katika Sodoma. Tazama, wao wote waliuendea Ulawiti, ulimwengu. Nadhani mmoja wa wasimamizi wa sinema aliweka picha muda mchache uliopita, nami niliiona; hiyo ilikuwa Sodoma. Ikiwa utawahi kuiona na hamna kitu kingine cho chote ila hiyo, itazame. Ilikuwa hakika picha nzuri ya Nchi ya Amerika siku hizi—Hollywood, vivyo hivyo hasa, aina ile ile ya mavazi na kila kitu walichofanya wakati huo, michezo ya ulevi wa kupindukia na kila kitu kinginecho—kundi lililojitenga la watu wa kidini, linalojiita la kidini.

¹⁵⁴ Tazama, na Sodoma ilikuwa na shahidi. Na alikuwa ni mtu aliyeitwa Lutu, aliyekuwa tu mpwake Ib—Ibrahimu. Sasa, Ibrahimu hakuvingia katika Sodoma. Yeye na kundi lake—yeye alikuwa na kundi kubwa pamoja naye, la kutosha kupigana na wafalme dazani moja pamoja na majeshi yao; kwa hivyo yeye alikuwa na kundi kubwa. Naye alikuwa ameketi nje pale chini ya mwaloni siku moja wakati kila kitu kilikuwa kinamwendea kombo; hakuna aliyehusika naye, lakini yeye alikuwa angali akishikilia ahadi hiyo. Tazama sasa, kwa makini, kabla hatujafunga. Wakati alikuwa bado amaketi pale, kukashuka watu watatu wakitembea kumjia. Wawili wao walikwenda Sodoma na kuhubiri Injili kwa wale waliotoka—kwa Lutu. Sivyo? Lakini Mmoja alikaa na Ibrahimu. Tazama, yule aliyekaa pamoja na Ibrahimu alikuwa Mungu Mwenyewe; na wale wengine wawili walikuwa Malaika wajumbe.

¹⁵⁵ Sasa, kule Sodoma hawakufanya miujiza yo yote, ila tu kuwapofusha, na kuhubiri Injili kila wakati hupofusha watu.

¹⁵⁶ Sasa tazama Utaratibu wa siku hizo. Kunalo kanisa la kawaida. Kila mara katika utatu [kama nilivyosema usiku uliopita] Mungu huwakilishwa. Pale kulikuwako Wasodoma. Walutu, na Waibrahimu. Ni hali ile ile usiku huu, ulimwengu ukikaa tu hivyo!

¹⁵⁷ Hebu niwaulizeni kitu fulani. Tazama utaratibu huu sasa. Ibrahimu alimwita huyu aliyeongea naye, *Elohim*. Neno la Kiebrania *Elohim* maana yake ni Yule aridhishaye kwa vyote. Yeye yule aliye wa Milele—*Elohim*, Mungu Menyewe.

¹⁵⁸ Hapo mwanzo...1 ilisema, “Hapo mwanzo, Mungu...” Chukua neno la Kiebrania pale—samahani lile neno la Kiyunani, “Hapo mwanzo *Elohim* aliumba mbingu na nchi.”

159 Yeye yuko hapa, Mwanzo, karibu ile ya 23 hapa... Yeye alisema...? ...Kuanzia au karibu ile ya 20... Yeye alisema... Na yeye aliita jina la mtu huyu *Elohim*. Mbona yeye alifanya hivyo? Mungu akiwakilishwa katika mwili wa kibinadamu, aliyekei na Ibrahimu kula kitoweo cha nyama ya ndama, akinywa maziwa, na kula mikate fulani—Mungu Mwenyewe—na akatowekea papo hapo mbele ya Ibrahimu!” Lakini Yeye alimpa Ishara. Tazama, na Ishara hiyo ilikuwa ya kwamba Yeye alikuwa amegeuza mgongo Wake kuelekea hemani. Na kumbuka Ibrahimu jina lake lilikuwa Abram u siku chache hapo kabla, na Sara alikuwa Sarai hapo kabla—S-a-r-a-i, ndipo S-a-r-a na A-b-r-a-m-u kuwa I-b-r-a-h-i-m-u. Ibrahimu maama yake ni baba wa mataifa.

160 Sasa, chunguza hapa kwa makini, na tutaona utaratibu wa ile saa tunayoishi sasa, kama Yesu alivyotuambia tutazame utaratibu huu. Tumeona ile mingine yote sahihi,—sasa hebu tuone ule Uzao wa Kifalme. Ni utaratibu upi wanaopaswa kuona.

Sasa, Mtu huyu alisema, “Ibrahimu, mke wako Sara yuko wapi?”

Na Ibrahimu alisema, “Yeye yumo hemani, nyuma Yako.”

161 Sasa, Yeye hajawahi kumwona kamwe. Yeye alijua kuwa jina lake lilikuwa Ibrahimu? Yeye alijua jina la mke lilikuwa S-a-r-a? “Ibrahimu, mke wako Sara yuko wapi?”

Na Ibrahimu alisema, “Yeye yumo hemani, nyuma Yako.”

162 Na Yeye alisema, “Mimi (Mimi, neno la kumtaja mtu)—nitawazuru kulingana na ahadi. Mke wako atapata mtoto. Umenisadiki Mimi, sasa nitalitimiza.”

163 Na Sara hemani nyuma Yake (akidukiza au kudoya, chochote mkiitacho), alisikiza akiwa hemani, naye akasema akachea kimoyomoyo na kusema, “Sasa, mimi, mwanamke mkongwe nilivyo, niwe na raha na bwana wangu naye pia ni mzee sana, zaidi ya umri wa miaka mia moja! Mbona, hili halijatendeka kwa miaka mingi, mingi sana.”

164 Na Mtu yule, M-t-u, akiketi pale na akila katika mwili wa kibinadamu, akinywa na kula kama mtu wa kawaida mwenye vumbi mavazini mwake, na alikuwa na vumbi miguuni Mwake na Ibrahimu akaisafisha—Mungu, Mwenyewe, alitazama hapa na pale naye alisema, “Mbona Sara alicheka nyuma hemani, akisema hili?” Yeye alijua, angetambua mawazo ya Sara hemani nyuma Yake. Sivo?

165 Sasa, wakati yule Mzao wa Kifalme wa Ibrahimu alipokuja ulimwenguni, je, alionyesha Ishara gani? (Mwana wa Adamu) Simoni alimjia siku moja, Andrea alimleta. Yeye kasema, “Jina lako ni Simoni, wewe u mwana wa Yona.” Yeye kasema... mwaona, hilo lilimfanya awe mwamini.

¹⁶⁶ Filipo akaenda na kumkuta Nathanieli; akarudi na kusema, “Njoo umwone Mtu tuliye mpata—tumempata: Yesu wa Nazareti, mwana wa Yusuifu.”

¹⁶⁷ Yeye alisema, “Sasa ngoja kidogo. Je, kitu cho chote kizuri kingetoka kwa ukichaa huo?”

Yeye alisema, “Njoo uone.”

¹⁶⁸ Kwa hivyo Filipo alipokuja katika Uwepo wa Yesu pamoja na Nathanieli, Yesu akamtazama pale na kusema, “Tazama, Mwisraeli kweli kweli, ndani yake hamna hila.”

Yeye akasema, “Rabi, ulinijua lini?”

¹⁶⁹ Yeye akasema, “Kabla Filipo hajakuita, ulipokuwa chini ya mtini, nilikuona.”

Yeye kasema, “Rabi, Wewe u Mwana wa Mungu! Wewe u Mfalme wa Israeli!”

Wakati mwanamke yule kisimani, katika hali yake ya zinaa, alikuja (onyesho dogo kitu fulani kama hicho) kuteka maji, Yesu alikuwa amewatuma wanafunzi kwenda kununua “chakula”. Naye mwanamke alipokuja kuteka maji, Yeye akamwambia, “Nipe maji ninywe, mama.”

¹⁷⁰ Yeye kasema, “Si desturi kwenu kusema hayo. Tuna ubaguzi hapa. Sasa, ninyi Wayahudi hamhusiki nasi Wasamaria; hatuhusiki nanyi kwa lo lote.”

¹⁷¹ Yeye alisema, “Lakini mama, kama ungejua yule unayeongea naye, ungeniuliza nikupe maji. Nitakupa maji usije ukayateka hapa tena.”

¹⁷² Yeye alipata hali yake ilivyokuwa, jinsi ilivyokuwa. Yeye alisema, “Mlete mume wako na mje hapa.”

Kasema, “Sina mume ye yote.”

¹⁷³ Yeye alisema, “Umesema kweli. Umekuwa na watano, na yule unayeishi naye sasa si wako.”

¹⁷⁴ Yeye kasema, “Bwana, naona kuwa wewe u nabii! Twajua Masihi ajapo Yeye atatuonyesha mambo haya.”

Yesu alisema, “Mimi ndiye!”

¹⁷⁵ Kwa hayo yeye alikimbia mjini na kusema, “Njoooni muone Mtu aliyeniambia mambo niliyoyatenda. Je, si huyu ni Masihi yule?”

¹⁷⁶ Tazama, Yeye alifanya hilo mbele ya Wayahudi na Wasamaria, lakini hajafanya kumwe kwa Mataifa. Mataifa, sisi watu, tulikuwa makafiri katika siku hizo (mataifa yale mengine), tukibeba rungu mabegani mwetu, tukiabudu sanamu; hatukumtarajia Masihi ye yote. Yeye huwatokea tu wale wanaomtarajia, nasi yatupasa tuwe tukimtarajia! Lakini wale wanaodai wanamtafuta, lile kanisa lenyewe, walipoona hayo

yakitendeka, wao walisema, “Yeye ni shetani; yeye ni mnajimu, Beelzebuli!”

¹⁷⁷ Na Yesu alisema kuwa dhambi hiyo wangesamehewa kwa kuwa Yeye hakuwa amekufa bado, lakini wakati mmoja Roho Mtakatifu atakuja na kufanya mambo yale yale, na kunena tu neno moja dhidi Yake hautasamehewa kamwe. Hiyo ni siku hizi, ambapo kila neno yapasa liunganike pamoja. Nena neno dhidi Yake, halitasamehewa katika dunia hii wala dunia ijayo.

¹⁷⁸ Huyu alikuwa Mzao wa Kifalme wa Ibrahimu. Na hapa huyo Mzao wa Kifalme wa Ibrahimu (ambaye alikuja kwa ajili ya kutambulishwa kwa yule Mtu akiketi pale pamoja na Ibrahimu) amekuja kuthibitisha kuwa ni Mungu yule yule aliyeahidiwa na katika siku hizi, kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma, ndivyo itakavyokuwa Mwana wa Adamu atakapokuja, anapojifunua Mwenyewe kama Mwana wa Adamu! Amina! Leo ni siku ya Maandiko hayo kutimia.

¹⁷⁹ Tazama utaratibu tulio nao leo. Tazama kanisa lile ambamo Mwana wa Mungu. . . Tazama siku ya utusitusi; tazama unabii wote. Sasa, jambo la ajabu—wageni wetu wamekaribia basi, ikiwa utaratibu hauna budi kuwa kama ulivyokuwa Sodoma.

¹⁸⁰ Palikuwapo watu watatu waliokuja—watu mashuhuri watatu waliotumwa toka Mbinguni, tutakubali hilo—watu watatu; Mmoja aliketi na Ibrahimu. Wao wote walianzia hapo, lakini Mmoja alikaa pamoja na Ibrahimu na wengine wao waliingia Sodoma. Sivyo? Na Ibrahimu alikuwa na jina lililogeuzwa, toka Abram hadi kuwa Ibrahimu. Kweli? Hakuna wakati hata mmoja historia—kanisa la ulimwengu limewahi kuwa na mhubiri wa Injili mwenye jina linalomalizikia na h-a-m hadi siku hizi—Billy G-r-a-h-a-m. Sivyo? G-r-a-h-a-m herufi sita. I-b-r-a-h-i-m ni herufi saba, lakini G-r-a-h-a-m ni herufi sita, ambazo ni ulimwengu—mwanadamu. Mwaona?

¹⁸¹ Tazama kile kimetokea leo toka kwa wale wajumbe waliotoka Mbinguni. Je, kunaye mwanadamu duniani anayehubiri toba kwa udhahiri kama Billy Graham? Je, kunaye mwanadamu ambaye amekuwa na ushawishi juu ya watu kama Billy Graham? Hakujawako kamwe mtu kimataifa. Lo, Billy Sunday na wengineo walikuwako humu Nchini Amerika, lakini Billy Graham anajulikana ulimwenguni kote. Oneni ambapo yeye anaitania?—toka Sodoma! Naye ana kundi lake limeshirikishwa pale pamoja na kanisa la Kipentekoste—Oral Roberts.

¹⁸² Na je lile kundi la Wateule? Ni aina gani ya Ishara wanayopaswa kuona? Wanapaswa wawe na nini? Haleluya! “Kutakuwako Nuru wakati wa jioni!” Leo Maandiko haya yametimia! Leo ahadi za Mungu zimetimia. Twajua hilo kuwa Kweli. Yeye yuko hapa usiku huu kama alivyokuwa wakati huo.

¹⁸³ Sasa, kuihubiri...Kama nilivyosema kitambo kidogo, ukihubiri cho chote na iwe ni Kweli ya Injili, basi Mungu lazima aithibitishe. Sivyo? Sasa ikiwa ni hivyo, na hebu Mungu aliyeandika Neno, hebu Mungu aliyefanya unabii ule, hebu na Mungu aliye Mungu wa Neno atokee na kuthibitisha kuwa Yeye yuangali Mungu!

¹⁸⁴ Kama Eliya alipokwea mlima akitazama—Elisha alienda akimtazama Eliya, yeye alisema, “Nataka fungu mara mbili.” Na lile joho lililokuwa juu ya Eliya likaanguka juu ya Elisha. Yeye alishuka chini na kukunja blanketi hiyo mara mbili na kupiga ule mto na kusema, “Mungu wa Eliya yuko wapi?” Na jambo lile lile lililotendeka kwa ajili ya Eliya, lilitendeka kwa ajili ya Elisha. Na Injili ile ile, nguvu zile zile, Mwana wa Adamu yule yule aliyekuwako jana, yupo leo, na atakuwako milele! Waebrania 13:8. Je, unaliamini?

¹⁸⁵ Sasa, nawaulizeni. Siwezi kuwa Yeye, lakini Yeye yuko hapa. Sisi ni wabebaji tu. Baadhi yenu watu mlioko pale wagonjwa na wanaoteseka (mnaojua kuwa siwajui, hebu Mungu sasa, ikiwa naweza kujinyenyekeza mwenyewe kutosha...), wewe omba na kumwuliza Mungu.

¹⁸⁶ Sibahatishi...Hakuna kadi ya maombi jengoni, iko? La, mimi si...Hatukutoa kadi zo zote za maombi. Tutakuwa na mkutano wa maombi—au kuponywa kwa wagonjwa kanisani. Lakini wewe omba, nawe wajua kuwa mimi ni mgeni kabisa kwako. Mwaona...Mwanijua, Jeffersonville! Sitaki watu toka Jeffersonville wafanye hivyo; nataka watu toka mbali na hapa mahali pengine. Tuone kama Mungu bado hufunua. Tuone kama Yeye yuangali yule jana, leo na hata milele.

¹⁸⁷ Fanya kama vile mwanamke yule alifanya. Yeye alipita na kusema, “Namwamini Mtu huyu.” Yeye alikuwa anatokwa na damu naye akasema, “Kama tu ningegusa upindo wa vazi Lake naamini nitapona.” Sivyo? Kwa ajili ya imani yake, siku hiyo Maandiko yale yalitimia. Yeye aliwaganga waliovunjika moyo, “Niliponya wagonjwa na viwete.” Alipogusa vazi Lake na akatoka nje na kuketi chini, Yeye aligeuka na kusema, “Ni nani aliyenigusa?”

¹⁸⁸ Angejuaje katika umati huo mkuu wa watu (labda mara thelathini zaidi ya tulio nao usiku huu, maelfu yao)—Yeye alijuaje? Yeye alisema, “Ni nani aliyenigusa?” Yeye hakusema hayo kwa kusema tu, Yeye alisema hayo kwa kuwa ilikuwa ni kweli. Na Yeye alisema, “Nani aliyenigusa?” Moja kwa moja, Yeye alitazama na kumwona mwanamke yule maskini, alipokuwa ameketi au kusimama, hali yoyote aliyokuwa—akamwambia kutokwa kwake na damu kulikwa kumekwisha. Huyu alikuwa ni Yesu jana; na huyo ndiye Yeye leo.

¹⁸⁹ Mwaamini hilo? Sikujui; Mungu akujua. Lakini una maumivu ubavuni mwako yanayokusumbua. Hiyo ni kweli.

Unaketi pale na kuomba juu yake. Je, mimi ni mgeni kwako? Sisi tu wageni mmoja kwa mwingine; simama wima kama ndivyo. Sikujui. Mtu huyu papa hapa pembeni, kijana huyu. Una koo baya pia. Naam. Unaomba juu yake; una wasiwasi kuhusu kitu fulani. Yakupasa uondoke mkutanoni, kwa kuwa wewe u mhudumu. Una shughuli fulani unazohitajika uzishughulikie. Naam. Waamini Mungu ajua wewe u nani? Mchungaji, Bw. Smith, sasa waweza kwenda na uponywe; Yesu Kristo akuponya. Kwenda mkutanoni mwako; koo lako halitakusumbua. Yeye alimgusa nani?

¹⁹⁰ Mtu yule anayeketi nyuma kule anaugua. Yeye ana kivimbe kwenye pafu lake la kushoto. Yeye ha—yeye hatoki hapa. Umekuwa mfanyi kazi katika migodi ya madini. Naam. Mimi ni mgeni kabisa kwako; ikiwa hilo ni kweli, pungu mkono wako. Kivimbe kile kiko kwenye pafu lako la kushoto, nawe unajitayarisha kwa kupasuliwa moja kwa moja. Sivyo? Hutoki hapa, unatoka nje ya mji. Unatoka Virginia. Naam. Je, waamini Mungu ajua u nani? Bw. Mitchell (naam), kwenda nyumbani na upone. Yesu Kristo akuponya. Mwulize mtu huyu; sijawahi kumwona maishani mwangu. Yeye alikuwa amaketi pale akiomba. Leo Maandiko haya . . .

¹⁹¹ Hapa kuna bibi anayeketi hapa nyuma yangu, kama Sara alivyokuwa hemani. Yeye anamwomba bintiye, Simama. Binti yule hayuko hapa; yuko mbali. Binti yule ana . . . yuko kama vile mwanamke yule alivyomjia Yesu aliyekuwa na bintiye aliyepagawa vikali na pepo. Mwanamke yule ni— msichana aliyepagawa na pepo. Yeye hayuko hapa; yeye anatoka—wewe unatoka Carolina ya Kaskazini. Waamini hilo, na hilo ni Kweli, sivyo? Bi. Orders, waweza kwenda nyumbani. Ukiamini kwa moyo wako wote, utamkuta binti yako kama yule alivyokutwa zamani za Yesu Kristo katika siku zilizopita; kasema ingekuwa hivyo.

¹⁹² Leo Maandiko haya—ile ishara ya Sodoma, ile ishara ya Mzao-Maalum, ile ishara ya kanisa la kawaida—leo Maandiko haya yametimia kati yenu! Je, unaliamini? Je, utamkubali sasa hivi kama Mwokozi Mponya wako? Simameni kila mmoja wenu na kusema, “Nakubali uponyaji wangu; namkubali kama Mwokozi wangu; namkubali kama Mfalme wangu.” Kila mmoja asimame kwa miguu yake.

¹⁹³ Leo . . . Sikizeni marafiki. Yeye aliyasoma Maandiko yale, akarudisha Biblia hiyo kwa kuhani yule, na kasema watu wote walimkazia macho. Naye akawatazama na kusema, “Leo Maandiko haya yametimia.”

¹⁹⁴ Nimesoma Maandiko, kukiwa na shuhuda dazani au zaidi kuwa tunaishi katika siku za mwisho, kizazi kile kitakachomwona Yesu Kristo akirudi duniani. Nami nawaambia usiku huu tena, leo Maandiko haya yametimia machoni penu!

¹⁹⁵ Ninyi katika Tucson, ninyi katika California, ninyi katika New York, kwenye simu hizi, leo Maandiko haya yametimia machoni penu! Hebu tufurahi na tupige shangwe, kwa kuwa ile arusi ya Mwana-Kondoo i karibu, na Bibi-arusi wake—Bibi-arusi Wake amejifanya tayari!

¹⁹⁶ Hebu tuinue mikono yetu na kumtukuza Yeye, enyi watu wote. Mungu awabariki.



LEO MAANDIKO HAYA YAMETIMIA SWA65-0219

(This Day This Scripture Is Fulfilled)

Ujumbe huu uliohubiriwa na Ndugu William Marrion Branham, uliotolewa hapo awali katika Kiingereza mnamo Ijumaa jioni, Februari 19, 1965, katika Ukumbi wa Shule ya Sekondari Ya Parkview Junior kule Jeffersonville, Indiana, Marekani, umetolewa kwenye kanda ya sumaku iliyorekodiwa na kuchapishwa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©2014 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org